

**SHULE YA SEKONDARI AHMES**  
**KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA TARAJALI**  
**KAZI YA LIKIZO**

1. .Kwa kutumia mifano,eleza maana ya istilahi zifuatazo
  - i. Mawasiliano
  - ii. Lugha
  - iii. Sauti nasibu
  - iv. Ala za sauti
  - v. Neno
  - vi. Sentensi
  - vii. Sarufi
  - viii. Fasihi
  - ix. Lugha fasaha
  - x. Lafudhi.
2. Lugha ni sauti za nasibu.Thibitisha kwa kutumia hoja za msingitatu (03).
3. Lugha fasaha huundwa na misingi mikuu mine.Taja misingi hiyo.
4. Taja na fafanua tanzu kuu nne za sarufi.
5. Nini hasara za kutotumia lugha fasaha? Taja hasara tano.
6. Katika lugha ya Kiswahili neno linaweza kuwa na maana zaidi ya moja.Taja maana mbili kwa kila maneno yafuatayo
  - i. Kata
  - ii. Mbuzi
  - iii. Paka
  - iv. Panda
  - v. Korongo .
7. a). Kamusi ni nini?
  - b). Taja na fafanua sehemu kuu tatu za kamusi.
  - c). Taja na fafanua aina kuu tatu za kamusi.
  - d). Nini umuhimu wa picha na michoro katika kamusi? ( Hoja 5)
8. Eleza dhima kuu tano za lugha.
9. Taja sifa na tabia sita za lugha.
10. Andika barua kwa mwalikmu wako wa somo la Kiswahili ukimweleza jinsi ulivyofurahia likizo.